# MSAMIATI WA TAKATAKA

**Msamiati wa maneno yanayohusu takataka na udhibiti wa takataka.**

**3Ks**
Njia fupi ya kusema 'Punguza, Tumia tena na Sarifu',pengine maneno muhimu matatu katika udhibiti wa taka. Katika kitabu tunaongezea dhana na Kukataa na Kufikiri tena!

**Takataka zinazooza**
Taka ambayo inaweza kuvunja vunwa au kuoza kwa kawaida wakati kushambuliwa na wadudu wadogo, bakteria na vimelea. Mifano ni pamoja na chakula na takataka za bustani. Aina nyingine ya takataka huitwa takataka zisizooza.

**Takataka hatarishi**
Takataka zenye uwezekano wa kudhuru binadamu, na vitu vyengine vyenye uhai na mazingira. Inahitaji kutupwa kwa uangalifu. Mfano wa taka hatarishi ni betri na friji na friza.

**Shimo jaa**
Taka nyingi huzikwa katika mashimo makubwa katika ardhi yaitwayo majaa. Maeneo yetu mengi ya majaa hivi sasa yamejaa taka na hatuna sehemu nyengine ya ardhi iliyobora yakuweka majaa mengine.

**Maji taka/maji machafu**
Maji maji yenye mchanganyiko wa maji ya mvua na vituvilivyooza ambavyo hutirika kwenye kwenye mashimo jaa.

**Taka**
Taka (kawaida ni karatasi, plastiki na gilasi) kutupwa katika mazingira, badala ya kuwekwa katika debe la taka au kituo chengine cha takataka. Si taka zote ni takataka lakini takataka zote ni taka.

**Maliasili**
Vitu vya matumizi ya binadamu ama vinavyokuja kutoka kwenye dunia yetu kwa mfano, maji, mafuta au madini.

**Taka za vitu vyenye uhai**
Taka inayotokana na mimea na wanyama. Taka nyingi za vitu vyenye uhai zinafanywa na chakula lakini vyanzo vingine ni takataka za bustani.

**Uchafuzi wa mazingira**
Kuweka sumu au vitu nyingine madhara katika mazingira.

**Malighafi**
Rasilimali za msingi zinazotumika kufanya vifaa na bidhaa. Kwa mfano, malighafi kwa ajili ya plastiki ni mafuta.

**Usarifishaji**
Usarifishaji ina maana ya kutumia ktu kilichokwishatumika na kutengeza kpya. Hii inaweza kuhusisha kugeuza kifaa kikuukuu katika kifaa kipya cha kitu kile. Vinginevyo, kifaa kinaweza kusarifiwa katika kitu tofauti kabisa.

**Kupunguza**
Kupunguza maana ya epuka kuzalisha takataka katika nafasi ya kwanza na ni jambo zuri zaidi kufanya kuliko kutumia tena au kusafu tena. Mifano ya kupunguza takataka ni pamoja na kununua vitu ufungaji wake ni mdogo na sio kubadilisha kitu mpaka kuwe na mahitaji ya lazima.

**Rasilimali**
Kwa ujumla neno ni vitu na vifaa ambavyo tunavipata kutoka katika ardhi. Rasilimali inaweza kugawanywa katika njia mbili. Rasilimali zilizofanywa upya ni zile ambazo zinaweza kuchukua nafasi yake wenyewe kwa muda mfupi kwa mfano maji au nishati ya jua. Rasilimai zisizoweza kufanywa upya haziwezi kamwe kubadilishwa au kuchukua muda mrefu sana wa kuchukua nafasi yake, kwa mfano makaa ya mawe na mafuta.

**Kutumia tena**
Kutumia tena ina maana kukitumia kitu tena, ama kwa lengo lile lile au kwa kitu tofauti kabisa. Mfano kurudisha chupa za soda kwa muuzaji kukarabati vifaa vya umeme wakati zinapokuwa hazifanyikazi badala ya kuyatupa.

**Takataka = Takataka = Taka**
Kitu chochote tunachofikiria hatuna tena matumizi nacho na hivyo kukitupa mbali. Maneno haya yote matatu yana maana moja.

**Endelevu**
Hii ina maana ya kutafuta njia ya kukidhi mahitaji ya kizazi cha sasa bila kuharibu mazingira au kuzuia vizazi vijavyo kutokana na kuwa na uwezo wa rasilimali za kutosha.

**Taka za sumu**
Taka zenye sumu sumu kwa binadamu au vitu vyenye uhai..